Universiteit Leiden
The Netherlands

# Tracing inclusivity: Contribution of the Dutch private sector to inclusive development in Kenya. Case study of Unilever Tea Kenya Ltd., the flower sector and Lake Turkana Wind Power project

Kazimierczuk, A.H.

**Citation**

Kazimierczuk, A. H. (2020, October 22). *Tracing inclusivity: Contribution of the Dutch private sector to inclusive development in Kenya. Case study of Unilever Tea Kenya Ltd., the flower sector and Lake Turkana Wind Power project*. Retrieved from https://hdl.handle.net/1887/137215

| | |
|---|---|
| Version: | Publisher's Version |
| License: | Licence agreement concerning inclusion of doctoral thesis in the Institutional Repository of the University of Leiden |
| Downloaded from: | https://hdl.handle.net/1887/137215 |

**Note:** To cite this publication please use the final published version (if applicable).

Cover Page

Universiteit Leiden

Leiden University
Repository

The handle http://hdl.handle.net/1887/137215 holds various files of this Leiden University dissertation.

**Author**: Kazimierczuk, A.H.
**Title**: Tracing inclusivity: Contribution of the Dutch private sector to inclusive development in Kenya. Case study of Unilever Tea Kenya Ltd., the flower sector and Lake Turkana Wind Power project
**Issue date**: 2020-10-22

# Muhtasari

## I. Utangulizi

Tasnifu hii inachunguza uwezekano wa mchango wa sekta ya kibinafsi ya uholanzi na mchango wa sera za maendeleo za sekta ya kibinafsi ya uholanzi (PSD), kwa maendeleo ya kijumla nchini Kenya katika sekta tatu: Kilimo cha majani chai,maua na nishati mbadala.Ni sehemu ya mradi mkubwa wa utafiti uitwao "Biashara ya kimataifa ya Uholanzi,Serikali ya Uholanzi na kukuza ajira yenye tija katika eneo la Afrika kusini mwa jangwa la Sahara: utafiti wa kulinganisha nchini Kenya na Nigeria." Mradi huu ulikuwa sehemu ya ajenda ya utafiti wa jukwaa la maarifa ya sera za maendeleo ya pamoja (INCLUDE), iliyosimamiwa na wizara ya mambo ya nje kupitia NWO-WOTRO.

Kwa kusudi la utafiti huu,maendeleo ya kijumla (ID) hueleweka kwa mapana kama maendeleo ya kunuia kupunguza umaskini na usawa (INCLUDE, 2019b: 5) na inachukuliwa kwa vipimo kiuchumi,tamaduni za kijamii,anga,kiikolojia na vya kisiasa(Bebbington, 2013; Gupta, Pouw, & Rostonen, 2015). Tasnifu hii pia inatambua umuhimu wa kutofautisha kati ya matokeo ya maendeleo ya pamoja na michakato ya maendeleo ya pamoja (INCLUDE, 2013; Kiislamu, 2019; Rocha Menocal, 2017b).

Ongezeko la hamu kwa wazo la maendeleo ya pamoja kwa mwongo uliopita kwa maeneo ya masomo na kisiasa ni matokeo ya kutambulika kwa vikundi maskini ambavyo havijanufaika vilivyo kati ya matokeo ya maendeleo kutoka kuendelea kiuchumi kwanza haswa katika eneo la kusini mwa Afrika mwa jagwa la Sahara (AfDB, 2015; Altaf, 2019; AUC/OECD, 2018; de Kemp & Lobbrecht, 2018; INCLUDE, 2019b). Kuendeleza maendeleo ya kijumla ni kiini cha chanzo cha malengo ya maendeleo bora (SDGs), ajenda ya maendeleo ya kimataifa ya mataifa ambao ni wanachama wa umoja wa kimataifa katika 2015 (Gupta & Vegelin, 2016; Osakwe & Moussa, 2017). Ili kupata ID kama ilivyo kwa ajenda ya SDG, sekta ya kibinafsi ilitambulika kama lengo kuu la washirika wakuu wa kimkakati (UN, 2015). Kuzingatia kuendelea kwa utambuzi wa nafasi ya sekta ya kibinafsi katika sehemu ya michakato ya maendeleo, washiriki wengi wa nchi za shirika la kusaidiana kiuchumi na maendeleo (OECD) imekuwa ikiendeleza ratiba ya sekta ya kibinafsi (PSD) kama mojawapo ya msaada rasmi wa maendeleo (ODA), kati yao ni taifa la Uholanzi. Serikali ya Uholanzi imekuwa ikiendelea kusaidia katika sera na kuanza kutia nguvu sekta ya kibinafsi na maendeleo ya kiuchumi kwa nchi zinazoendelea tangu mwanzo wa pande zote mbili zinazosaidia. Dhana mahsusi iliyopo kwa sera za Uholanzi (PSD) (za 2015 lakini kifumbo, pia imejitwalia tangu 1960s) ilikuwa "mwandamo mzuri wa sera, maendeleo ya kiuchumi na kibiashara ni nguvu ya kupunguza umaskini" (MFA , 2015b ) na kampuni za zinazounda (uzalishaji) kazi za uholanzi na kuongeza CSR katika taifa 'mwenyeji' na la 'nyumbani'. Hata hivyo, ushahidi wa kusaidia huu ukisi umekuwa hafifu.

Sekta ya kibinafsi imechangia maendeleo ya pamoja kwa njia mbalimbali lakini sanasana imechangiwa wazi kwa kuleta ajira (uzalishaji) na kusaidia umoja wa kijamii kwa kutoa programu za majukumu la shirika la kijamii wanalofanya kazi nalo (CSR) (Goris & Vrancken, 2018; Gupta & Vegelin, 2016; Kapstein, 2008; Kolk & Lenfant, 2018; Kontinen & Spierenburg, 2008; Kourula, Pisani, & Kolk, 2017; Osakwe & Moussa, 2017; Porter & Kramer, 2011; Scheyvens, Banks, & Hughes, 2016; UN, 2015; Utting & Marques, 2010). Ajira ya uzalishaji imetambulika kama ajira inayotoa chumo ya kutosha kwa kuruhusu wanaoitegemea kwa kiwango cha matumizi kwa mapato ya kadri (Szirmai, Gebreeyesus, Guadagno, & Verspagen, 2013). Hata hivyo,mbali na makubaliano ya kawaida kuwa sekta za kibinafsi pamoja na kampuni za kimataifa zifanyazo kazi katika mataifa yanayoendelea yanajukumu muhimu la kufanya kupunguza umaskini na usawa. Hadi sasa kuna uhusiano unaoonekana kati ya shughuli za sekta za kibinafsi za kimataifa katika nchi zinazoendelea na mchango wao katika maendeleo ya kijumla (Katika masuala ya matokeo na michakato) imefanyiwa utafiti kiasi wa kitaaluma. Majadiliano yanayolenga kufafanua jukumu hili mara nyingi hukosa fikra za kutosha kwa muktadha muhimu wa kihistoria, kisiasa na mambo ya kitaasisi na kwa hivyo inabaki kuwa si sawa (Boyle & Boguslaw, 2007; Fortanier & Kolk, 2007; Kolk & Lenfant, 2018; Kolk, Rivera-Santos, & Rufín, 2018; Meyer, 2004; Oetzel & Doh, 2009; Utting

& Marques, 2010). Hata hivyo utafiti zaidi unaonyesha muktadha zaidi na kufunua muktadha na mienendo ya shughuli za kimsingi za sekta ya kibinafsi ya kimataifa, Mataifa yanayoendelea,haswa katika Afrika inahitajika (de Haan, 2015; Kolk, Kourula, Pisani, & Westermann-Behaylo, 2020; Kolk & Lenfant, 2018; Lashitew & Van Tulder, 2017).

Tasnifu hii inaangazia kuleta mchango wa kupunguza pengo la maarifa kwa:

- **Kwanza**, kuchunguza uwezekano wa mchango wa sekta ya kibinafsi ya Uholanzi katika nchi ya Kenya kwa vigezo tano vya maendeleo ya jumla (kiuchumi, tamaduni za kijamii, maswala ya anga, Kiikolojia na kisiasa); zote kwa masharti ya matokeo na michakato.
- **Pili**, kuchunguza dhana ya nadharia iliyowasilishwa na serikali ya Uholanzi katika sera zao za maendeleo ya PSD ambazo zilianzisha utaratibu wa kawaida kati ya ongezeko la ushirikiano wa kiuchumi uliochochewa sera za maendeleo (misaada ya nchi mbili,mauzo ya nje,na kuhusika kwa moja kwa moja kwa sekta ya kibinafsi ya Uholanzi kwa nchi zinazoendelea, na uundaji wa ajira (yenye tija), na hivyo kuchangia maendeleo ya kijumla katika nchi zinazoendelea.

Hii itafanyika kwa kusoma sehemu tatu muhimu za sekta ya kiuchumi nchini Kenya na kuchambua pamoja ni hizi sekta na jukumu la Uholanzi MNCs na sera za maendeleo za Uholanzi PSD ya MNCs 57 ya Uholanzi yaliyokuwa Kenya mwaka wa 2014, msingi wake ulidhaniwa kuwa mchango muhimu wa kila sekta moja kwa moja kwa kuunda ajira nchini. Sekta zilizochaguliwa na uchunguzi kifani kama ifuatavyo:

- Sekta ya Kilimo cha majani chai: Kisa cha kampuni ya majani chai ya Unilever (UTKL) (iliangaziwa katika sura ya 3);
- Sekta ya kilimo cha maua (Uchambuzi mpana wa sekta) (iliangaziwa katika sura ya 4);
- Sekta ya Nishati mbadala: Kwa kina uchunguzi kifani wa mradi wa nishati upepo wa ziwa Turkana (LTWP) (iliangaziwa katika sura ya 5).

Uchambuzi wa uchunguzi kifani unatambua kuwa uongozi, uchumi wa kisiasa na vipengee vya makazi ya siasa unachangia jukumu muhimu kwa kutengeneza michakato ya maendeleo na kutengeneza au kuzidisha vikwazo ili kufanikisha matokeo ya maendeleo ya pamoja (Awortwi & Dietz, 2019; Hickey, Sen, & Bukenya, 2015; Rocha Menocal, 2017a).

## II. Mchango wa maarifa na mazoezi

Utafiti huu umefanywa kwa wakati unaofaa na una umuhimu kwa wasomi na kwa ajenda ya mjadala wa maendeleo endelevu ya sababu tatu za kimsingi:

1. Itachangia kwa umuhimu wa matini ya sekta ya kibinafsi ya kimataifa kwa kufikia maendeleo ya pamoja na jukumu la sera za kuunga mkono kwa taifa 'mwenyeji' na la' nyumbani'.
2. Itaboresha mjadala ikizingatia umuhimu wa uchumi wa siasa na maendeleo ya michakato katika makazi ya siasa.wakati tu makazi yamejadiliwa kwa michakato ya nguvu inayohusisha vikundi vilivyochaguliwa vya watendaji wa mikakati, pamoja na serikali ya MNCs. Kwa sababu michakato hii hufanyika kisiri badala ya njia ya kawaida.Utafiti huu utaziangazia kama njia za kawaida.
3. Itathibitisha umuhimu wa tofauti kati ya vipimo tofauti vya ID, vilevile kati ya matokeo ya maendeleo ya umoja na upekee na michakato inayoangazia maendeleo ya sekta ya kibinafsi nchini Kenya,haswa yanayoangazia mashirika ya kigeni.Pia itafanya hivyo angalau kwa kisa cha mashirika yanayofanya kazi kwa kilimo cha majani chai,maua na sekta ya nishati mbadala nchini Kenya. Sekta ya kibinafsi inauwezo wa kuleta matokeo ya kijumla kwa uchumi, tamaduni za kijamii, sehemu ya anga, vipimo vya ikolojia, walakini (siasa) mchakato unaopelekea matokeo haya huwa ndefu na ya kipekee (wakati mwingine ya kawaida).

## III. Maswali ya utafiti

Swali kuu la utafiti linaloongoza tasnifu hii ni:

*Ni mchango upi wa sekta za kibinafsi za Uholanzi zinazofanya kazi katika sekta za kilimo cha majani chai, maua na nishati mbadala nchini Kenya na maendeleo ya pamoja katika nchi hiyo?*

Maswali yanayounga mkono ni kama yafuatayo:

- Ni sababu zipi kuu na zinazosaidia michakato au kuzuia uchambuzi wa sekta za kibinafsi za kiholanzi nchini Kenya ili kufanikisha matokeo ya maendeleo ya kijumla.
  - o Ni michakato ipi kuu na matokeo yepi ya maendeleo ya kilimo cha majani chai, maua na sekta ya nishati mbadala nchini Kenya?
  - o Michakato na matokeo haya ni ya aina gani (ni ya pamoja au ya kipekee)?
  - o Ni majukumu yepi ya sekta za kibinafsizilizochambuliwa katika katika michakato hii?
  - o Ni mchango upi wa sekta za kibinafsi zilizochambuzi katika kufanikisha matokeo ya maendeleo, haswa kupitia (uzalishaji) kutoa nafasi za ajira na programu za ushirika wa jukumu la kijamii (CSR)?
- Ni jukumu lipi la serikali ya Uholanzi kwa sekta ya kibinafsi na maendeleo ya sera kwa kusaidia sekta ya kibinafsi kuwa pamoja kwa maendeleo ya nchi zinazoendelea (haswa Kenya)?

## IV. Eneo la utafiti

Kenya ilichaguliwa kuwa nchi ya kuangaziwa kwa sababu imekuwa mojawapo ya nchi zinazopokea msaada kutoka uholanzi na uwekezaji kati ya nchi shirika za Uholanzi barani Afrika (Kazimierczuk, Dietz, & Vink, 2016). Nchi ya Kenya ndiyo inayoongoza kiuchumi katika eneo la Afrika Mashariki lakini pia inajulikana kwa utata wa kisiasa unaojitokeza kwa kujihusisha kindani kwa wanasiasa walio kwa shughuli za biashara. Mwisho Kenya inajulikana kama mojawapo ya nchi za Afrika ambazo zimepitisha au mbinu wazi na mkakati wa taifa katika shughuli za kampuni za kimataifa. Kwa hivyo ,ilikuwa ya kuvutia, pia kuchunguza jinsi mtazamo huu ulivyoshawishi makubaliano ya biashara za kimataifa kwa lengo la sera katika kukuza ajira ya uzalishaji na maendeleo ya pamoja kwa nchi (ASCL, UoN, & KAM, 2014).

Utafiti wa nyanjani ulifanywa kati ya Oktoba-Novemba 2015, Juni-Oktoba 2016, Agosti 2017, na Januari-Februari 2019, katika baadhi ya sehemu, ikiwamo Nairobi, Limuru, Naivasha, Timau, Kericho na katika baadhi ya sehemu la Laisamis jimbo.

## V. Mbinu

Ili kuelewa miktadha na mifumo inayotakikana katika kila sekta,utafiti huu ulitumia utafiti wa maelezo muundo na mbinu ya mchakato wa kufuatilia ubora wa juu. Kwa nadharia-jenzi na uwezo wa upimaji wa nadharia. Ili kupata mchakato huu wa kufuatilia ulijumuishwa na uchunguzi kifani, ambao mchanganyiko wa mbinu zilitumiwa. Ili kuhakikisha kuwa kuna uwezo wa pamoja wa sekta zilizochaguliwa zimefanyiwa utafiti wa kutosha. Mchakato wa kufuatilia uchunguzi kifani uliongozwa na mtazamo uliowasilishwa na Dekker (2017), sehemu iliyounganishwa na kuwekwa na Betsema, & Zoomers (2017), na kutengenezwa kwa muktadha wa sekta ya kibinafsi katika bara la Afrika. Kulingana na maoni yao, umaskini fulani unaangaziwa ili kuelewa miktadha (pia wa kihistoria) ambayo kampuni za kibinafsi hufanya kazi kutambua na kueleza mwingiliano wao na mandhari ya kisiasa, kijamii na kiuchumi na jinsi mwingiliano huu hushawishi asili ya matokeo ya jinsi zifanyavyo kazi. Zaidi, mifumo na michakato inayopelekea nguvu za kijumla ama kipekee kwa kila sekta iliyochunguzwa huzingatiwa. Mwishowe jaribio pia limefanywa ili kuwekwa kwa hifadhi ya maandishi wapi na vipi kwa kazi zilizotengenezwa, vipi na mbona manufaa yake kwa sekta ya kibinafsi zinavyosambaa kwa jamii. Kwa kufanya hivyo, tasnifu hii inamwongoza msomaji kwa safari ya kihistoria kupitia hatua kuu za uchumi wa Kenya katika Karne ya 20 na 21 ilivyounganika na usawa wa maagizo ya maendeleo ya kimataifa inavyoonekana kupitia kwa

sekta tatu zilizofanyiwa utafiti: Sekta ya kilimo cha majani chai, maua na nishati mbadala kwa michakato ya maendeleo husika.

## VI. Matokeo

*i. Kuhusu mchango wa sekta ya kibinafsi ya Uholanzi inayofanya kazi kwa sekta ya kilimo cha majani chai, maua na sekta ya nishati mbadala nchini Kenya na maendeleo ya kijumla katika nchi hiyo.*

### Matokeo ya jumla

Kwa kutumia mbinu ya kufuatilia mchakato wa nadharia-jenzi kwa kutahini uchunguzi kifani na nishati mbadala, tasnifu hii inaonyesha kuwa Uholanzi MNCs nchini Kenya zaweza kuchangia kichanya kwa kiuchumi, tamaduni za kijamii, sehemu ya anga, ikolojia na hata vipimo vya kisiasa vya maendeleo ya kijumla. Matokeo haya yanathibitisha kuwa sekta ya kibinafsi ina mantiki kwa matokeo ya kazi zake na kufanya mchango mkubwa kwa vipimo vya kiuchumi. Mabadiliko kuelekea kwa kufahamu zaidi na shughuli endelevu (kimataifa lakini haswa Uholanzi) imechangia kwa matokeo ya kijumla ya tamaduni za kijamii, vipimo vya ikolojia. Wakati mwingine shughuli muhimu ama michakato hufanyika wakati huo kwa matokeo ya kijumla au kipekee.

Hata hivyo, ilichunguzwa kuwa matokeo chanya hayakufanyika moja kwa moja na hayakufika kipimo chake cha juu sawia. Zilipatikana kwa faida ya sekta ya kiuchumi na kufikia watu walioweza kufanya kazi kwa sekta hizi wakiishi karibu na kampuni ama wale ambao waliweza kufaidika kutoka kwao kama watumizi. Matokeo hayo ni nadra yakifuatana na awamu ya maendeleo ya sekta (isipokuwa kwa LTWP), kuonyesha muda ulihitajika wakati huo (sehemu zote), pia kupewa motisha wakurugenzi wakuu (sehemu zote) na sera za kindani zilizojitolea (LTWP) ili kufikia vikundi kama hivyo. Sera zinazounga taifa 'mwenyeji' au la 'nyumbani', vile vile shinikizo la kimataifa lilikuwa la maana,haswa kwa mashirika yanayoshughulikia mauzo ya nje. Hii inaonyesha umuhimu wa sekta za kibinafsi za kimataifa kwa kufanikisha maendeleo ya kijumla, lakini pia jukumu la sera za kuunga mkono taifa 'mwenyeji' au la 'nyumbani'.

### Biashara katika mwelekeo wa kisiasa.

Hakuna biashara ya mbali au mbaya ambayo imepatikana kwa matokeo ya kiuchumi,tamaduni za kijamii na vipimo vya ikolojia. Hata hivyo, kuingizwa kwa sehemu anga ilivyoopuzwa ni swala la LTWP lililopea viongozi wa kawaida sauti na wanasiasa ikipelekea matokeo ya pamoja katika vipimo vya kisiasa. Walakini, ni kwa vipimo vya kisiasa ambapo biashara halisi huangaziwa. Kweli ilibainika kwa muktadha wa Afrika na Kenya, uwepo na utekelezaji wa uwazi katika mfumo wa kisheria na motisha katika sekta ya nishati mbadala ni muhimu kuvutia wawekezaji wapya lakini haitoshi pekee yao. Pia kinachoongezea ni uwezekano wa kujadili mbinu moja kwa moja na serikali. Hii si tu dalili ya nishati mbadala, lakini inaonekana sawa kwa visa vingine pia.

### Maendeleo ya 'kawaida'

Katika sekta zote zilizotafitiwa, karibu matokeo yote ya kijumla ya: kiuchumi, tamaduni za kijamii, masuala ya anga, vipengele vya kiikolojia, yalifuatwa na michakato mirefu ya kipekee ya siasa na shirika tendaji la kampuni za Uholanzi lililotafitiwa pamoja na mataifa, taifa na serikali za mtaa. Michakato hii haikuwa tu ya kipekee mbali pia ya kawaida iliyofanyika faragani kati ya makundi yaliyochaguliwa kwa uangalifu na waliohusika. Hivyo basi nikatumia neno maendeleo ya 'kawaida'. Katika kesi zilozotafitiwa mchakato wa 'kawaida' hufanyika wakati wa hatua za awali za uanzishwaji wa sekta binafsi za kigeni zilizochunguzwa katika nchi zinazoendelea. Michakato hii haikuwa tu ya kipekee lakini ilikuwa muhimu

na pia (kufikia sasa) sehemu isiyoweza kutengwa na michakato ya maendeleo ambayo ilisababisha matokeo ya kijumla. Hii inahusiana na majukumu ya mtu binafsi na mikakati ya watendakazi wanaofanya kazi katika muktadha maalum kuhusu mataifa, taifa na kiwango cha mtaa. Matokeo haya yalithibitisha umuhimu wa kutofautisha kati ya vipimo tofauti vya maendeleo ya kijumla, vya kipekee na jumla lakini pia matokeo ya maendeleo ya 'kawaida' na michakato kuhusu sekta za maendeleo ya kibinafsi nchini kenya, haswa wakati inahusisha kampuni za kigeni.

Umuhimu wa uchumi wa kisiasa na uchambuzi wa mikataba ya kisiasa katika muktadha wa historia

Ili kuelewa utata wa kisiasa na 'ukawaida', ni muhimu kuweka uchambuzi wa kampuni zilizotafitiwa katika muktadha wa kihistoria (Utting na Marques, 2010). Historia kama hii ya uchumi ni wazi kuwa iliathiriwa na uchumi wa kisiasa na mikataba ya siasa ambayo huamua kama lengo la maendeleo ya kijumla yatapatikana au la. Lengo la msingi la serikali ya muungano ni kubaki katika (Whitfield & Buur, 2014), serikali hii inaweza zaidi kutekeleza mabadiliko muhimu iwapo inakabiliwa na shinikizo kutoka (ikiwezekana) vikundi vyenye mamlaka katika jamii (Awortwi & Dietz, 2019; Bates & Bates, 2005; Berendsen, Dietz, Nordholt, & Van der Veen, 2013; Vlasblom, 2013). Sekta za kibinafsi zinaweza kukuonyesha kuwa ni vikundi vyenye mamlaka sanasana katika nchi ambapo mahusiano ya uangalizi ni makubwa na yenye nguvu. Nchi na ustawi wa biashara zinauhusiano wa karibu (Akinyoade & Uche, 2018; Booth, Cooksey, Golooba-Mutebi, & Kanyinga, 2014; Booth & Therkildsen, 2012). Wakati uo huo sekta za kibinafsi ziko chini ya matakwa ya serikali hiyo ya muungano. Kama ustawi wa makundi haya mawili yanafanana, itaweza kusababisha matokeo muhimu ya maendeleo. Hii inaonyesha umuhimu wa kufikiria kuhusu uchumi wa kisiasa na uchambuzi wa mikataba ya kisiasa katika muktadha wa historia wakati wa majadiliano ya shughuli za sekta za kibinafsi za kimataifa katika nchi zinazoendelea ili kuelewa vizuri jinsi athari ya shughuli zao zinavyoweza kuathiri uchumi wa nchi husika.

ii. *Kuhusu majukumu ya sera za maendeleo ya sekta ya kibinafsi ya kiholanzi katika kusaidia sekta binafsi za kiholanzi kuhusika zaidi katika shughuli zao katika mataifa yanayoendelea(haswa nchini Kenya).*

Sura 2 inafafanua uhakiki kuhusu sera za maendeleo za kiholanzi (kutoka 1949), kwa kusudi la kukuza maendeleo ya sekta za kibinafsi (PSD). Hii huonyesha kuendeleza mbinu za uholanzi kwa maendeleo ya sekta za kibinafsi kama njia ya kukuza biashara za kiholanzi na mauzo ya nje katika mataifa yanayoendelea. Kwa kufuata njia ya uchunguzi kifani wa nadharia katika muktadha wa tatu wa utafiti uliochaguliwa, tasnifu hii hufafanua zaidi uwezekano wa kudhibitisha dhana kuu juu ya sera za PSD za kiholanzi za sekta ya ukulima wa majani chai, maua na nishati mbadala nchini kenya. Dhana hii na nadharia imeletwa na serikali ya kiholanzi katika sera zao za maendeleo ikaanzisha utaratibu wa kawaida kati ya kuongezeka kwa ushirikiano wa kiuchumi na sera za maendeleo na kutoa nafasi za ajira (zenye tija) hivyo kuchangia maendeleo ya kijumla katika nchi zinazoendelea. Kudhibitisha uhalali wa dhana ya sera iliyojaribiwa lazima mtu atambue utaratibu sahihi wa moja kwa moja kati ya sera za maendeleo za kiholanzi na mchango wa sekta za kibinafsi za kiholanzi kwa maendeleo ya pamoja katika sekta za utafiti nchini kenya.

Kwa bahati mbaya data iliyokusanywa haionyeshi utaratibu wa moja kwa moja kati ya sera za maendeleo ya kiholanzi na ufadhili uliotolewa na kampuni za kiholanzi katika sekta zilizotafitiwa na mchango wao katika maendeleo ya pamoja nchini kenya. Kwa sababu hiyo ni vigumu kudhibitisha uhalali wa dhana ya sera zilizojaribiwa. Hili ni jambo lenye utata mkubwa ambalo linahitaji mbinu ya

utaratibu zaidi ambayo haiwezi kufuatwa katika utafiti huu. Walakini, viunganishi maalum vimeangaliwa kati ya sera za kinyumbani na za kampuni zinazofanya biashara katika nchi husika: sera za maendeleo za kiholanzi kati ya mambo mengine muhimu, yalihimiza biashara za kiholanzi kuwekeza katika mataifa yanayoendelea ikiwemo Kenya.

Uwepo wa kampuni za kiholanzi nchini Kenya katika sekta tatu ni muhimu kwa taifa – Ukulima wa maua, majini chai na nishati mbadala- imekuwa na jukumu muhumu katika uanzishwaji wa sekta hiyo na maendeleo. Uwepo wao au kutokuwepo kumechangia nafasi za ajira katika taifa husika (ingawa mara nyingi haitoi nafasi za kazi kikamilifu) na kupitia shughuli zao za CRS (ingawa imegawanyika au sio ajira zenye tija kabisa) zimesaidia kwa kiwango fulani jamii iliyohusika ambapo wanafanyia kazi. Walakini katika kesi zilizochunguzwa (sura 3-4) ni kampuni chache tu zilizofaidika kutoka msaada wa kifedha wa moja kwa moja kupitia programu za PSD za kiholanzi na sanasana katika awamu ya mwisho ya maendeleo ya sekta. Ni LTWP pekee iliyopokea msaada kama huo katika awamu ya maendeleo. Baadhi ya mipango iliyofadhiliwa na serikali ya kiholanzi katika sekta zilizochunguzwa zilikuwa muhimu katika sekta nzima. Kwa mfano:

- Kwa upande wa UTKL, mipango endelevu ya biashara (IDH) ilianzilisha nyanja mbalimbali za masomo ya wakulima (FFS), ambayo ilifanya kazi ya kupitisha maarifa na kujumuisha wakulima wadogo wa majani chai.
- Katika ukulima wa maua, msaada kwa baraza la maua Kenya (KFC) kupitisha ujumbe wa kiwango kinachohitajika cha taifa cha kilimo cha maua na mapambo (KS 1758 sehemu 1) ilikuwa na jukumu la kuhakikisha ujumuishaji mkubwa wa mazingira kwa kuchochea hali inayofaa zaidi ya mazingira na matumizi salama ya kemikali katika sekta nzima.
- Kwa upande wa LTWP, mchango wa moja kwa moja wa serikali ya uholanzi kwa ujenzi na uboreshaji wa barabara na pia katika mradi wenyewe kupitia mkopo uliotolewa na kampuni ya kufadhili maendeleo ya kiholanzi (FMO) haikuwa muhimu tu kwa ukulima wa upepo lakini pia ilikuza eneo lililokuwa limepuuzwa kwa muda mrefu. Kwa hivyo imechangia kupunguza kutengwa kwa eneo kwa kujumuisha baadhi ya vikundi vya wenyeji kiuchumi na kisiasa.

Ikumbukwe hata hivyo, kwamba hakuna moja kati ya mipango hiyo ilikuja bila kiwango fulani cha ubishi.

## VII. Hitimisho

Kuhitimisha, tasnifu hii hufafanua kwa mapana maendeleo ya kijumla kama “maendeleo ambayo yanayolenga kupunguza umaskini na ukosefu wa usawa” (INCLUDE, 2019b: 5). Kwa muktadha wa sekta tatu zilizochunguzwa (kilimo cha chai, maua na nishati mbadala) hapa nchini inathibitishwa kuwa maendeleo ya pamoja yalitokana na shughuli za sekta za kibinafsi zilozoweza kuchangia katika umaskini na upungufu wa usawa (uchumi,kitaduni, masuala ya anga, ikolojia na siasa) lakini sio kwa uwezo kamili wa jumla. Ni muhimu kukumbuka kwamba kampuni za kibinafsi zinafanya kazi katika mazingira maalum na lazima pia kutumia hali zilizopo. Mifumo hii haijumuishi kikamili. Haitawezekana katika muktadha wa uendeshaji wa sekta binafsi (na kwa kawaida ikiwezekana) ilimuradi maendeleo yanayotokana na soko yabaki na yaliyoingia katika itikadi ya sera za mageuzi ya soko.

Shinikizo la kimataifa, wakfu wa ndani au sera za kitaifa, vilevile motisha ya kibinafsi ya wakurugenzi wasimamizi ni muhimu kwa kuhimiza ujumuishaji. Kimsingi, matokeo ya kijumla yanaweza kupatikana ikiwa masilahi ya sekta za kibinafsi na kuunganisha serikali ya muungano. Hii inahitaji mazungumzo ya muda mrefu ya ‘kawaida’ kati ya vikundi vya watendaji wa kimkakati pamoja na sekta za kibinafsi. Matokeo ya kijumla (ilimuradi tu watatoa fursa kwa watendaji waliohusika) lakini makubaliano yaliyoafikiwa huwa nadra kukosoa utawala uliopo badala yake ndio wanawaunga mkono.

Sera za PSD za kiholanzi zilikuwa muhimu kuhimiza wanabiashara kuekeza ughaibuni lakini mchango halisi kwa maendeleo ya jumla nchini Kenya hayawezi kupimika. Historia ya sera za maendeleo ya

kiholanzi, kupendekeza suluhisho kadhaa katika suala la jinsi ya kutumia maarifa na ujuzi wa nchi kufanya kazi kwa niaba ya mikoa iliyoendelea kwa mipango yenye faida huchochea maendeleo ya uchumi. Diplomasia ya uchumi basi inapaswa kuzingatia kukuza sera ambazo zinahimiza maendeleo ya pamoja. Zaidi ya hayo, msaada uliopeanwa kwa sekta za kibinafsi katika mataifa yaliyoendelea ni muhimu lakini sera za PSD huhitaji kuangalia kinachohitajika na sekta za kibinafsi katika muktadha fulani, ili kuchangia kiasi cha maendeleo ya jumla nchini. Ili haya kufanyika,ni muhimu kupata maarifa ya wanabiashara wa kiholanzi waliona uzoefu katika kufanya biashara nchini. Wakati mipango ya PSD inapaswa kuanzisha mafunzo ya mifumo ya ndani ya wafadhili wa sekta za kibinafsi kutambua changamoto na mienendo inayoendelea na kuzoea miktadha husika. Mwisho, sera kama hizi na programu haipaswi kufanya kazi katika ombwe badala yake itoe msaada kwa nchi husika, shirika la kisekta, vyama vya wafanyakazi na shirika la asasi za kiraia kwa pamoja kuunda mazingira bora ya biashara.

## VIII. Mapendekezo

Kulingana na utafiti huu, mapendekezo yafuatayo yalitolewa kwa serikali ya uholanzi kwa ajili ya kuongeza mchango wa sekta za kibinafsi za kiholanzi katika maendeleo ya jumla nchini kenya na mataifa yanayoendelea.

### Kiwango cha zoezi

- Kutambua kuwa sekta za kibinafsi zina uwezo wa kuchukua jukumu katika kufanikisha maendeleo ya kijumla ilimuradi sera zinazounga mkono nchi husika ziwekwe. Kwa hivyo, kusisitiza kuhusu kukuza sera za maendeleo ya kijumla katika taifa husika. Inaweza kufanywa kupitia juhudi za diplomasia za kiuchumi za balozi za kiholanzi.
- Kutoa msaada kwa kampuni mpya za kiholanzi zinazoingia soko la kenya kutoka balozi la kiholanzi, vilevile ushauri kutoka kwa wafanyabiashara walio na tajriba ya kufanya biashara nchini.
- MNCs za kiholanzi zinahitaji kurekebisha mtindo wao wa biashara ili kuhimiza matokeo ya maendeleo. Matokeo kama haya yanafaa kutoa nafasi za kazi na mipango bora zaidi ya CSR inayozidi miundo ya kisasa. Kampuni zinapaswa pia kufanya juhudi za kuelewa kwa undani muktadha wa eneo lao na washika dau.
- Kutambua umuhimu wa kutoa msaada kwa sekta za kibinafsi katika mataifa yanayoendelea katika maendeleo na ukomavu wake. Msaada wa kitaaluma na maendeleo ya utaratibu wa vipimo vya taifa. Wakati uo huo kuunga mkono ushirika wa sekta za kenya, vyama vya wafanyikazi na mijadala ya kitaifa ya umma na ya kibinafsi katika kuimarisha sauti za sekta binafsi na asasi za raia katika kubuni na kukuza mikakati ya uchumi wa taifa kwa mfumo wa kitaifa unaojumuisha zaidi.
- Kutoa msaada kwa maendeleo na uchunguzi unaofanywa vilevile utafiti wa umma ili kuimarisha kupitisha maarifa kwa ujumla kwa changamoto zilizopo utawalani katika taifa husika na kuwezesha kuhusishwa kwa sekta zilizo na uwezo.

### Kiwango cha programu

- Muktadha na wakati ni jambo muhimu, muktadha wa historia, kijamii na uchumi, haswa msingi wa uchumi wa kisiasa na mahusiano ya kiutawala, miundo ya kujumuisha na kutojumuisha sekta za kibinafsi katika nchi zinazoendelea. Programu zinazosaidia katika maendeleo ya sekta binafsi zinapaswa kuzingatia mienendo hiyo (ikiwepo michakato ya 'kawaida') na ipasavyo

kuwaingiza katika mipango yao na matokeo tarajiwa. Uhitaji wa uwazi Zaidi (‘kawaida’ kwa sasa) michakato inaweza kuhitajika.

- Kuhusisha utaratibu sahihi wa mafunzo katika mipango ya PSD, ambayo ingeiruhusu kampuni na wafadhili kutambua na kuzoea haraka mbinu/njia bora ili kuafikia malengo ya kawaida.
- Kuongeza juhudi za kukuza njia kamili ya kushughulikia athari ya vyombo vya habari vya PSD. Zaidi ya hayo, utafiti kuchambua mkusanyiko wa biashara za kiholanzi katika nchi zinazoendelea inapaswa kufanywa ili kulenga maeneo bora ambayo hayatumiki.
- Kutoa msaada mkubwa na kutoa motisha kwa kampuni zinazowekeza kwenye masomo na kukuza maendeleo ya wafanyakazi wao zaidi ya hayo, kutoa msaada kwa kampuni ambazo zinaajiri watu wenye ulemavu (kuongezea nafasi za kazi kwa kikundi hicho).

### Kiwango cha sera

- Sera za PSD na programu lazima zielewe jukumu na mapungufu ya sekta za kibinafsi katika maendeleo ya taifa katika nchi husika. Kutambua kuwa mchango wa sekta za kibinafsi kwa maendeleo ya jumla yanayoonekana zaidi katika vipengele vya uchumi na vinaweza kusababisha ujumuishaji kamili katika vipengele vyote chini ya mfumo wa sasa wa uchumi wa dunia. Pia kutambua kwamba wakati unahitajika kufikia matokeo ya pamoja.
- Kukuza na kuhimiza sera zinazoimarisha utaratibu sawa kati ya sekta za kibinafsi za serikali na asasi za kiraia. Serikali husika inafaa kufanya kazi ya kuunda mazingira bora ya biashara na mifumo ya kutosha ya uangalizi.
- Epuka sera zenye mwelekeo mmoja, sekta tofauti zinakabiliwa na changamoto tofauti na watendaji wanaohusika si kundi moja. Mahitaji ya sekta zote yachukuliwe kwa makini ili kuhakikisha ujumuishaji kamili.
- Kufanya uchunguzi zaidi kupima mawazo ya kimsingi ya sera za PSD kwa kutumia ‘mbinu ya kufuata njia’ kushughulikia changamoto zinazohusiana na kupata data nyanjani. Kampuni ambazo zitazingatiwa kwa utafiti kama huo zinapaswa kuwa tayari kushiriki kutoka mwanzo. Kampuni za kibinafsi zilizonufaika kutoka ufadhili wa serikali ya uholanzi zinapaswa kuhimizwa kushiriki katika utafiti kama huo.
- Kutambua uchumi wa kisiasa na sababu za makazi ya kisiasa katika mipango na sera za Kiholanzi, pia mawazo yao kuhusu nadharia zao za mabadiliko.